


MASHAHIDI

 Habari za jioni, marafiki. Ni furaha sana kuwa hapa usiku wa leo, kumtumikia Bwana. Hili limekuwa juma tukufu kwetu, haya majuma mawili yaliyopita. Ndugu Neville alinirudisha tu chumbani na alikuwa akizungumza nami, na kusema kwamba kulikuwa na zaidi ya waongofu mia moja, waliokuwa wamemjia Bwana; na karibu mabatizo hamsini, walibatizwa majini. Hilo lafaa. Sivyoy? Tuna furaha sana kwa ajili ya hilo.

² Tuna furaha kuwa na wageni malangoni petu usiku wa leo, na tunaomba kwamba Mungu atawabariki kwa wingi sana. Nasi tunataka kumshukuru kila mtu ambaye ameweka juhudi katika mkutano huu, kufanya jambo fulani kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

Tunataka kumshukuru Ndugu yetu Thom.

³ Na—na Ndugu Tom Merrideth na Dada Merrideth, na mtoto Merrideth hapa, wote wawili, na hao wote, kwa uimbaji wao, muziki; nasi bila shaka tunawakaribisha tena kwenye Maskani ya Branham wakati wowote. Wote wanaojisikia hivyo, semeni “amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ndugu Merrideth, unajua jinsi tunavyojisikia. Ndio kwanza nikutane na Ndugu Merrideth, hivi majuzi, naye amekuwa rafiki wa karibu sana.

⁴ Ndugu Neville kwa ninii yake, na Ndugu Merrideth, wote wawili, kwa mahubiri yao hodari, na kusimama karibu, na yote waliyofanya.

⁵ Ndugu Neville, tuna furaha kuwa nawe kama mchungaji wetu hapa, wa kanisa hili. Tunataka ujue kuwa upendo wetu wenye kilindi sana ni kwa ajili yako. Nami nina imani na Ndugu Neville; niliyafuatilia maisha yake ya nyuma. Nanyi mnaujua ule msemo wa kale, “Kuniishia mahubiri ni bora kuliko kunihubiria mamoja,” ukweli mwingi kwa hilo. Na kwa hiyo mimi—mimi nina furaha sana kwamba Ndugu Neville yuko hapa pamoja nasi, kuchukua kazi ya uchungaji wa kondoo hawa ambao ndio kwanza wameletwa zizini. Bwana Yesu ambariki ndugu yetu!

⁶ Na kwa mashemasi na . . . kila mtu, tunashukuru tu.

⁷ Tunaye Ndugu Kidd, naamini ndiye, na wengi wa wahudumu hao wengine mbalimbali, na Ndugu Hoover. Sijui kama Ndugu Hoover yuko hapa usiku wa leo, ama la, lakini amekuwa pamoja nasi na alibatizwa asubuhi ya leo.

⁸ Ndugu Beeler, rafiki yetu wa kale na mwenzetu safarini, katika Injili, kama mtaniwia radhi kwa kusema hivyo. Tuna furaha kuwa pamoja naye na ushirikiano wake. Anaandika ta—

taarifa za mikutano, na kadhalika. Naye atakuwa akiziishia tena na tena, kwa muda mrefu, nadhani.

⁹ Kwa hivyo tunamfurahia sana kila mtu, kwa...ninyi mlioimba nyimbo maalum, na kila kitu. Bwana Yesu awabariki, ndilo ombi langu.

¹⁰ Nimechoka tu kidogo usiku wa leo. Sijapata kupumzika sana. Jana usiku kulikuwa na mahubiri maradufu, na nikaingia karibu, kulala, yapata saa saba. Na kuamka tena asubuhi ya leo, mapema sana, na ibada ya mapambazuko, halafu shule ya Jumapili. Kisha, nikakaa ndani ya maji karibu saa mbili, nikibatiza.

¹¹ Maji hayo ni baridi. Sivyo, marafiki? Loo, hayo ndiyo maji baridi sana niliyopata kuona, niliyowahi kuhisi, hasa. Jamani, sijawahi...Nilikuwa nimekufa ganzi sana mpaka nikaninii tu...Sikujua kama nilikuwa nikipanda au kushuka, nikitoka mle.

¹² Kwa hiyo hata sikuchangamka nilipofika nyumbani, naye mke wangu akasema, "Chakula cha jioni kiko tayari." Ndipo nikaruka tu kwenye beseni kubwa la maji moto, ndipo kwa namna fulani nikapata joto kidogo; halafu nikavaa nguo zangu, nikaenda kwenye ibada ya mazishi.

Basi tukafanya ibada ya mazishi.

¹³ Ndipo nilipofika tu nyumbani, kulikuwa na simu ya dharura kutoka hospitalini, kwa hiyo ilinibidi nigeuke na kurudi hospitalini.

¹⁴ Sikupata chakula chochote cha jioni, kwa hivyo nilinini tu...Ndugu McSpaddin, kundi letu, tulikuwa huko na tukala chakula kidogo cha jioni, muda mfupi tu uliopita.

¹⁵ Kisha tukarudi sasa kwa ajili ya ibada ya jioni, na kumalizika kwa uamsho. Hakika tuna furaha sana kwa ajili ya haya majaliwa. Nimepwelewa tu na sauti kidogo, kwa hivyo mtanivumilia.

¹⁶ Nikasema, asubuhi ya leo, "Nitazungumza usiku wa leo, juu ya, 'Ishara kumfuata Mwaminio.'"

¹⁷ Sikujua, nilipoingia asubuhi ya leo, mbona, au jioni hii—hii, hasa, mpaka mmoja wa wadhamini hapa kanisani, aliposema, "Ndugu Bill, unakumbuka, usiku wa leo ni usiku wa ushirika."

¹⁸ Nikawazia, "Loo, jamani, sisi hapa tena sasa!" Kwa hivyo nikarudi chini, nikawazia, "Bwana, sasa nitazungumza juu ya nini?"

¹⁹ Nilikuwa na safu nzima ya Maandiko hapa, yaliyoandikwa, nami ningerejea mengi ya hayo, juu ya, "Ishara kumfuata mwaminio," kwa hiyo ilibidi nibadilishe hilo kidogo. Kwa hiyo sasa, labda, kwa hiyo tuna ibada ya ushirika, nasi tunatumaini ya kwamba mko pamoja nasi katika karamu hii kuu. Ni wakati

mzuri jinsi gani wa kula ushirika, mara baada ya ufufuo. Na wakati mzuri wa Roho Mtakatifu kushuka, pia, moja kwa moja katika majira yale yale sasa ambapo Roho Mtakatifu alishuka.

²⁰ Kwa hiyo, usiku wa leo, natumaini sasa sikuiipoteza tiketi hiyo. Sinema ya Billy Graham ya uinjilisti iko Louisville, nayo itakuwa ikionyesha *Mnara wa Mafuta wa Marekani*, tarehe ishirini Aprili, kwenye Ukumbi wa Makumbusho. Mimi. . . Waliniuliza, usiku wa leo, kama ningetangaza hilo, mmoja wa washirika wa Billy Graham, angelitangaza katika kanisa langu. Alinipa kadi yake. Kwa hiyo mimi. . . Ngingependa, kama mngeweza, kuiona hiyo, kama haiwasumbui. Nami ninaamini itakuwa nzuri. Alikuwa na sinema hii hivi majuzi, *Bw. Texas*, na wengi wenu mliiona hiyo, sinema nzuri sana, kweli. Wala sijawahi kuona hata mojawapo, lakini nimesikia maoni mengi sana juu yazo. Hiyo ni tarehe ishirini Aprili, kwenye Ukumbi wa Ukumbusho huko Louisville.

²¹ Na sasa, pia, ninaamini kutakuwa na uamsho utakaoendelea juma hili, kule—kule ukumbini pia. Kijana mwinjilisti fulani alikuwa kule akihubiri. Na ikiwa uko hapa karibu, na unaweza, najua wangeshukuru. Najua vile. . . Ninawaambia, laiti nisingekuwa na la kufanya, kutoka tu uamsho mmoja hadi mwingine. Hiyo ni kusema, napenda kuifuatilia mioto nipate joto. Nanyi je? Hilo ni jema.

²² Ndugu Merrideth, ulikuwa umewatangazia watu ambapo matangazo yako yanapoingia, na kila kitu? [Ndugu Tom Merrideth anasema, “Hapana, Ndugu Branham.”—Mh.] Vema, waweza kuja hapa na kufanya hivyo sasa hivi? Ndugu Merrideth atatangaza ninii yake. . . [Ndugu Merrideth atatangaza nyakati za kipindi chake cha kila siku cha redio.] Asante, Ndugu Tom.

²³ Na je, kuna mtu mwingine yeyote aliye na uamsho anaotaka kuutangaza, ama kitu chochote maalum, yeyote wa wahudumu? Nasi sikuzote tunafurahia kuwatambua ndugu zetu na huduma zao. Bwana awabariki sasa.

²⁴ Na sasa msisahau kukaa pamoja nasi, kama mnaweza, mara baada ya ibada hii, ibada ya kuzungumza, kwa ajili ya—kwa ajili ya ushirika na kutawadha miguu. Ni wangapi wamewahi kusikia habari za kutawadha miguu? Vema, hivyo, mko nyumbani tu hapa kama vile mfuko ulivyo kwenye shati. Sasa, tunaamini hilo kwa sababu Biblia, tunafikiri, inafundisha hivyo. Kwa hiyo la—laiti mngalibaki na kuwa pamoja nasi.

²⁵ Mnawakumbuka Wabaptisti wa mtindo wa kale kule Kentucky, jinsi tulivyokuwa tukila chakula cha jioni sakafuni? Nao wazee wangesimama na kuimba huo kama tulivyoimba kule kwenye mikondo ya kile kijito, (mnakumbuka?), “Neema ya ajabu, jinsi inavyosikika tamu!” Ndugu wote wanarudi chini ya miti yenye vivuli pale, nao wangeanza kutawadha miguu na kupiga makelele. Hao walikuwa Wabaptisti halisi. Hatukupeana

mikono sisi kwa sisi, kama ninyi Wabaptisti mnavyofanya siku hizi. Tulipigana mgongoni mpaka anapopita. Kweli walikuwa na kitu fulani. Tunapaswa kuwa na wengine wengi wa hao Wabaptisti, sivyo? Hiyo ni kweli.

²⁶ Na kwa hiyo bado tunakuadhimisha hapa, kutawadha miguu, nasi tungewatakeni muwe pamoja nasi, ikiwezekana, usiku wa leo. Kwa hiyo nitajaribu kuacha, kuzungumza tu, maana kidogo nimepwelewa na sauti. Kwa hiyo, niombeeni sasa.

²⁷ Na sasa nataka kusoma kidogo katika Agano Jipya, katika mlango wa kwanza wa Matendo Ya Mitume. Nadhani haya yanapaswa kuitwa Matendo ya Roho Mtakatifu katika Mitume. Ilikuwa ni jinsi Roho Mtakatifu alivyowafanya mitume watende, Yeye akiisha kuja. Sasa, katika kifungu cha 8, tunasoma jambo hili.

Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi...katika Yerusalemu, . . .Uyahudi, . . . Samaria, na hata pande za mwisho wa dunia.

²⁸ Na sasa, kwa dakika chache tu, ninataka kutumia somo la: *Mashahidi*.

²⁹ Na sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu, kinachofuata tu, kwa muda kidogo wa maombi, tafadhali.

³⁰ Sijui kama dada yetu angeweza kutupa sauti kidogo ya *Kaa Nami*, kitu kama hicho, dada, tafadhali.

³¹ Sasa, kila mtu hapa ndani aliye na haja sasa. Je, ungefanya tu jambo hilo lijulikane kwa Mungu, kwa mkono wako ulioinuliwa? Mwonyeshe tu Mungu, “Ni—nina haja, Bwana.” Nimeinua wangu, pia. Na abariki kila mmoja wenu, na awape shauku ya moyo wenu. Wakati kila mtu, kwa njia yake mwenyewe sasa, jinsi tu unavyoomba kanisani, hivyo ndivyo ninavyokutaka uombe.

³² Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja Kwako mwishoni mwa siku nyingine. Jua la kupendeza lililokuwa likichomoza asubuhi ya leo, sasa limetua na limeshuka, na mawingu yake meusi yameifunika anga. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya siku hiyo na kwa kumbukumbu tuliyokuwa nayo ya siku ile kuu ya ukumbusho wakati Yesu, Bwana, alipofufuka katika wafu.

³³ Kweli, kama vile maumbile yalivyo, ndivyo itakavyokuwa hivi karibuni, machweo ya wakati yanashuka. Haitachukua muda mrefu kabla ya kuwa giza kabisa. Wengi wataachwa hapa wapitie kipindi hicho cha wakati, jinsi ambavyo njaa na kiu ya uamsho wa mtindo wa kale kama ule ambao umekwisha.

³⁴ Mungu, ninamwombea msichana yule huko nje hospitalini sasa hivi, aliyekuwa kwenye ajali hiyo, iliyopasua moja ya mapafu yake; ikamrarua mumewe vibaya; akapondwa, akagandamizwa; moyo wake ukarushwa upande wa pili,

haiwezekani kabisa kwa madaktari. Je, waweza kuwa na huruma sasa hivi?

³⁵ Kumbuka, Bwana, ya kwamba Bw. Pritchard amelala pale, akihema, akifa. Kwa mtweto wa pumzi, alipokuwa akikifikia kihema cha oksijeni, alimpokea Kristo kama Mwokozi wake binafsi.

³⁶ Huko chini kwenye nyumba ya mazishi, leo, wakati akipiga magoti mle chumbani, maskini yule mwanamke mkongwe, umri wa miaka themanini na kitu, alisema hajawahi kumkubali Kristo kama Mwokozi wake binafsi. Na pale kwenye nyumba ya mazishi, kwenye mazishi ya mjukuu wake, akamkubali Kristo kama Mwokozi wake binafsi. Mungu na awe pamoja naye!

³⁷ Wabariki wale wote hapa Maskanini, Bwana, majuma haya mawili, waliomjia B- . . . Wewe. Kuwa pamoja nao. Wabariki wale waliobatizwa asubuhi ya leo. Jalia wakue katika neema na katika kumjua Bwana, hata wapate kukifikia kimo kamili cha Yesu Kristo, ndipo siku moja wanyakuliwe pamoja Naye katika wingu, kukutana na Yeye hewani, na milele wawe pamoja na Bwana.

³⁸ Wabariki wote walio hapa, usiku wa leo, Bwana. Na akiweko yeyote humu ndani ambaye bado hajakukubali Wewe kama Mwokozi wao, jalia hii iwe ndiyo saa ya uamuzi wao. Jalia waje kwa uzuri, unyenyekevu, na kumkubali Yeye kama Mwokozi wao binafsi. Tujalie, Bwana.

³⁹ Na sasa, kama maskini mtumishi Wako, asiyestahili, asiyefaa chochote, inaonekana kura imeniangukia kuumeza Mkate wa Uzima, kwa watu tena usiku wa leo. Bwana, ninaomba ya kwamba utasaidia, usiku wa leo. Jalia Roho Mtakatifu, utu wa tatu wa utatu, aje, alichukue Neno la Mungu, na kuliweka katika kila moyo, sawasawa na mahitaji yake. Halafu jalia limwagiliwe maji kwa imani, na lizae wingi wa matunda. Tujalie, Bwana.

⁴⁰ Tunakupenda, na tunakuamini na kukutumikia. Sasa pokea shukrani zetu, kwa maana tunaomba katika Jina la Bwana Yesu, Mwanao mpendwa. Amina.

⁴¹ Tunaanza, usiku wa leo, katika somo hili dogo, fupi la Neno la Mungu. Na wakati nikitamani kila mwaminio awe katika maombi, maombi ya kina, kwa ajili yangu sasa. Hakuna mtu anayeweza kulifungua Neno hili la Mungu. Tunaweza kuzivuta nyuma kurasa hizo, lakini, kulifungua Hilo, inahitaji Roho Mtakatifu. Mwanadamu hawezi kufanya hivyo. Hatuna uwezo huo. Yohana aliiona Biblia imewekwa Mbinguni, naye akasema, "Hapakuwapo na mtu Mbinguni, wala duniani, wala chini ya ardhi, aliyestahili hata kukitwaa kile Kitabu, kukifungua, ama kuifungua Mihuri." Ndipo basi akaona, "Mwana-Kondoo, kana kwamba amechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, Yeye akaja na kukitwaa kile Kitabu kutoka katika mkono wa kuume wake Yeye aliyeketi juu ya Kiti cha Enzi, akaifungua ile

Mihuri, na kukifungua kile Kitabu na kukifungulia watu.” Pia jalia aje, usiku wa leo, na kufanya vivyo hivyo.

⁴² Yesu hapa alikuwa akiwateua mitume Wake, kwa sifa za Roho Mtakatifu, kabla ya kwenda kuwa mashahidi. Na somo langu usiku wa leo ni, “*shahidi.*”

⁴³ Sasa, mahakamani, shahidi lazima ajue jambo fulani. Mtu yeyote tu hawezi kuingia na kuwa shahidi. Lazima iwe ni mtu ambaye anajua kitu fulani. Na hivyo ndivyo ilivyo tunapomshuhudia Bwana. Inahitaji mtu ambaye anajua kitu fulani.

⁴⁴ Basi Yesu akawazia, akasema haya, ya kwamba kabla hawajawa mashahidi Wake, “Ilibidi wangoje huko Yerusalemu hata walipovikwa Uwezo utokao Juu,” ndipo wangekuwa mashahidi, kote duniani; katika Yerusalemu, Uyahudi, Samaria, na hata pande za mwisho za dunia.

⁴⁵ Katika mahakama, kuna aina mbili za mashahidi ambao watasimama, yaani, wa jicho au wa sikio. Sasa, kama ukiketi chumbani na kuangalia kwa darubini, na kuona ajali, ushahidi wako, neno lako halifai kitu, kwa sababu ulikuwa ukiangalia kwa darubini. Huna budi kuwa pale pale, karibu, upate kujua kwa hakika kile unachozungumzia, kabla hujaweza kuwa shahidi. Inabidi usikie, au inakubidi kuona, kabla ya kuwa shahidi kwenye kesi ngumu mahakamani.

⁴⁶ Huwezi kusema, “Binti *Nanii* aliniambia, ama Bw. *Nanii*, ama Kasisi *Nanii* aliniambia.” Yeye ni shahidi, lakini wewe siye.

⁴⁷ Kwa hiyo, basi, hakuna mtu anayeweza hasa kushuhudia ufufuo wa Kristo, ila tu kwa Roho Mtakatifu. Huna budi kuwa shahidi binafsi, wewe mwenyewe; ukiwa hapo, ukijua jambo fulani juu yake, ukijua unachozungumzia.

⁴⁸ Na Mungu atusaidie tuone siku ambayo watu watakuwa tu kile walicho. Mnajua, mimi ni . . . Nasema hivi sasa kwa heshima zote. Sio jiji letu, lililojaa vilabu vya pombe haramu, ambalo linatudhuru. Hiki hapa kinachotudhuru, zaidi ya hayo yote, ni watu wanaokiri kuwa Wakristo wala hawaishi hivyo. Hicho ndicho, mnaona. Wao si shahidi wafaa.

⁴⁹ Hawawezi kushuhudia hadi wawe na tukio. Basi wanapokuwa na tukio, ndipo wanapokuwa shahidi, moja kwa moja, kwa sababu wamezaliwa mara ya pili. “Na mambo yote ya ulimwengu, mambo ya kale, yamepita, na mambo yote yamekuwa mapya.” Ndipo unakuwa shahidi wa Yesu.

⁵⁰ Yesu alijua, kabla mitume hawa hawajaweza kutoka na kuwa mashahidi wa kweli, kwamba iliwabidi kupata tukio la yale waliyokuwa wakishuhudia. Hilo si lingekuwa jambo zuri, leo hii, kama kila seminari ingefanya jambo lile lile, kama kila Mkristo angefanya jambo lile lile? Angekuja tu kanisani na kusema, “Sasa ninamkubali Yesu kama Mwokozi wangu binafsi.

Nitakaa papa hapa mpaka nipate ubatizo wa Roho Mtakatifu, kisha nitatoka niwe shahidi.” Mnaona? Mambo yangukuwa tofauti. Je, hamfikirii hivyo? Tusingekuwa na shuhuda hizo zilizolegea, zilizotawanyika.

⁵¹ Watu hushuhudia na kusema wao ni Mkristo, na kutoka nje na kuishi maisha mengine. Naye asiyeamini anaingia na kuona hayo, anasema, “Vema, angalieni pale! Hivyo ndivyo wao. . .” Naye ibilisi sikuzote atawaelekezea kidole, pia. Unaweza tu kutegemea hilo. Yeye ni mfanyabiashara. Wala usidharau uwezo wake na milki zake za kibiashara, kwa sababu anajua yote yanahusu nini.

⁵² Sasa, kabla hujaweza kuwa shahidi, kama nilivyosema, huna budi kujua jambo fulani. Kweli inakubidi kuwa shahidi.

⁵³ Mungu alikuwa na shahidi katika Agano la Kale. Mmoja wa . . . Mmoja wa mashahidi Wake wa kwanza alikuwa Nuhu. Nuhu alikuwa shahidi kwa sababu aliisikia sauti ya Mungu, katika onyo, ambalo, likimwambia gharika inakuja, na kwamba lazima ajenge safina. Na matayarisho ya safina hii yalikuwa yawe tayari mara moja, naye alipaswa kuandaa mahali kwa ajili ya kuwaokoa watu. Wote ambao wangeingia, wangeweza kuingia. Naye alikuwa shahidi wa Mungu.

⁵⁴ Sasa, jambo pekee alilojua, ni kwamba Mungu alikuwa amemwambia, ya kwamba kutanyesha. Ingawa haikuwa imewahi kunyesha juu ya nchi, lakini Mungu alisema itanyesha. Kwa hiyo ikiwa Mungu alisema itanyesha, basi hiyo ilimaanisha itanyesha. Kwa hiyo alikuwa shahidi wa Neno la Mungu. Na kwa hiyo alitwa, naye akatoka na kuandaa safina na kutayarisha vitu, kwa ajili ya mvua, kabla mvua haijaanza kunyesha. Halafu, kuna shahidi mwingine wa Mungu.

⁵⁵ Kulikuwa na watu fulani wakati mmoja, Wayahudi; kutoka kabila la Yuda, ambako walipata jina lao. Kwa sababu hawakutaka kufuata maagizo ya Mungu, wasingeshika amri Zake, Mungu alimwita Mfalme Nebukadreza aingie na kuwachukua mateka, awapeleke huko chini katika nchi ya Babeli. Wengi wetu tunaikumbuka ile hadithi ya kale inayojulikana sana juu ya vile walivyotundika vinubi vyao kwenye mwerebi, wala wasingeweza kuimba nyimbo za Sayuni. Ushindi wao wote ulikuwa umepotea, si kwa sababu Mungu alitaka kuwanyang’anya, lakini kwa sababu ya dhambi yao, iliyowatenganisha na Mungu.

⁵⁶ Hiyo ndiyo sababu, usiku wa leo, kwamba wengi wa Wakristo hawajapata ushindi, ni kwa sababu dhambi zao zimewatenga na baraka; wamekatiliwa mbali, huko nyikani mahali fulani, peke yao. Nayo mioyo yetu inaning’inia kwenye mwerebi uliao, kwa sababu hatuwezi kuzifurahia nyimbo za kanisa.

57 Nakumbuka zamani sana, tulipozoea kuingia humu. Wangukuwa wakicheza *Pale Chini Msalabani*, kwenye piano, kengele ilipokuwa ikipigwa, nao wakaingia. Kusingekuwa na angalau jicho moja kavu kanisani, kila mtu akilia, polepole, mtulivu. Ninapenda tu njia ya mtindo wa kale; Nguvu tulivu, tamu, za Roho Mtakatifu, zikitokea. Kabla hatujaweza kupata ufanisi wowote, hatuna budi kuvunjika, kwanza. Unajua, kama vile mfinyanzi, nabii alikuwa akishuka kwenye nyumba ya Mfinyanzi, akavunjwe, ili kufinyangwa tena. Nanyi mwajua, ikiwa hakuna kuvunjika, hakuna kufanywa upya tena. Inakubidi uvunjwe kwanza.

58 Na jinsi ambavyo, kama tu vile ardhi, kama utapata mazao, Ndugu Wright, inakupasa kulima shamba lako, kwanza, ulipasue yote vipande-vipande. Halafu upande mbegu yako, nayo itachipuka. Inategemea umepanda mbegu ya aina gani, basi, wakati imevunjika. Hivyo basi wakati mazao yananinii . . . shamba limelimwa kabisa, ni wakati wa kupanda mbegu.

59 Ndipo, hawa ndugu waliokuwa wameondoka katika nchi ya ahadi, wakashuka kuingia Babeli, walichukuliwa, kwa sababu dhambi zao zilikuwa zimewatenganisha na Mungu.

60 Na mimi ni wa mtindo wa kale vya kutosha kuamini, usiku wa leo, hili, kwamba wakati kanisa au mtu yeyote binafsi anapoanza kucheza na kucheza-cheza na ulimwengu, utakuwa na tukio lile lile; kumwacha Mungu, kuiacha ile Kweli. Nami ninaamini hilo. Na—najua kuwa hilo ni kweli.

61 Nimekuwa katika huduma sasa, miaka ishirini, na nimeona aina na namna zote mbalimbali kote ulimwenguni. Lakini ninawaambia, marafiki, mnaweza kudharauliwa, lakini napenda mkutano wa mtindo wa kale, uliovunjika.

62 Mtu fulani alipitia hapa, siku moja, na kusema, nilipokuwa nikihubiri hapa, kasema, “Je, mwanamke huyo . . . Billy, ungewezaje kuhubiri, na mwanamke huyo ameketi kule nyuma akifoka, akilia, akipiga mayowe ‘Amina?’”

63 Nikasema, “Labda hiyo ndiyo ilikuwa sababu kubwa ya mimi kuhubiri. Kweli. Naam.” Nikasema, “Kama yeye . . .”

64 Kasema, “Vema, hilo karibu lingeniua mimi, kama—kama nilikuwa nikijaribu kuzungumza, na mtu fulani akipiga makelele namna hiyo.”

Nikasema, “Hayakunisumbua, ndugu. Yalikuwa yakinitia moyo.”

A—akasema, “Je, alikuwa ni mwenye dhambi mbaya sana, ama kitu fulani?”

Nikasema, “La. Alikuwa Mkristo, aliyejazwa na Roho Mtakatifu.”

“Kisha analia?”

65 Nikasema, “Naam. Biblia ilisema, ‘Mtu aendaye zake, akilia, hakika atarudi tena, akileta pamoja naye miganda ya thamani.’”

66 Amina. Hiyo ni kweli. “Yeye atokaye kwenda kupanda,” mnaona, “na—na kuru- . . . kupanda machozi, bila shaka atarudi tena, akileta pamoja naye miganda ya thamani, akishangilia anaporudi.” Tanguliza mambo ya kwanza, kuvunja, kufanya upya; kisha uje ukishangilia. Amina. Vema.

67 Hawa wana wa Israeli walishuka kule chini, walikuwa chini ya mfalme mwingine. Sio. . . Mfalme wao mwenyewe alikuwa amehamishwa pamoja nao. Wakawa chini ya mfalme mwingine, mfalme katili, Mfalme Nebukadreza. Kwa hivyo siku moja, alisema, kwamba, “Ikiwa watu wowote. . .” Alipofanya, aliposimamisha sanamu kubwa huko makondenani, na kusema, kwamba, “Kila mtu ambaye hatainamia sanamu hiyo, hana budi kutupwa katika tanuru ya moto na kuteketezwa.” Ni m—mkataba wa jinsi gani uliofanywa, kwamba wavulana hawa wanapaswa kuchomwa moto, kila mmoja!

68 Na kulikuwako na watatu kule chini waliokuwa na majibu ya hapo awali ya maombi, walioitwa Shadraka, Meshaki, na Abednego. Waliigeuzia sanamu hiyo migongo yao. Nao wakasema, “Na ijulikane kwako, Ee mfalme. . .”

69 Nataka mtambue hili. Mungu anawataka mashahidi Wake wawe imara; si shahidi leo, na kesho yake hana msimamo.

70 Nilikuwa nikihubiri ibada ya mazishi leo, na kukemea kwa nguvu; mtu fulani akaniomba kuninii, akasema, “Nafikiri wengi wa hao watu walikuwa wenye dhambi, hawakuwa wamemkubali Kristo.” Nilidhani labda kidogo nilikuwa nimekemea vikali kupita kiasi.

71 Ndipo nilipokuwa nikitoka, kwe—kwenye gari la mtayarisha mazishi, alinyosha mkono akanipigapiga begani, akasema, “Mhubiri, nataka kukupongeza.”

Nikawaza, “Uh-loo.”

72 Akasema, “Hivyo ndivyo ninavyofikiri kwamba linapaswa kuhubiriwa.” Akasema, “Siipendi dini isiyo na msimamo.”

73 Nikawazia, “Jamani, kuna matumaini kwako.” Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, ambapo unaliweka hasa mahali pake. Hiyo ni kweli kabisa.

74 Ndipo hawa wana wa Israeli, hawa, Shadraka na Meshaki na Abednego, mashahidi wa Mungu.

75 Mungu hajawahi kuwa bila shahidi. Sikuzote ameninii. . . Sasa hapa ninawatakeni mlipate hili kwa karibu sana. Mungu hajawahi, wakati wowote, kuwa bila shahidi duniani. Sikuzote amekuwa na angalau mtu mmoja ambaye angeweza kuweka mikono Yake juu yake, aseme, “Huyo ni shahidi wangu.” Ilifikia kwa mtu mmoja, wakati mmoja; naye Ayubu alikuwa ndiye shahidi Wake pekee; na Ibrahimu n—nchini; lakini

Mungu alikuwa na shahidi. Mtu fulani atamshuhudia Mungu mahali fulani.

⁷⁶ Sasa, baada ya kitambo kidogo, tunataka kujua shahidi ni nini hasa, wa siku hii. Vema. Angalia.

⁷⁷ Watu hawa, walipokuwa wakishuka huko, walikataa kula vyakula vya mfalme, kunywa divai yake, nao wakakataa kuisujudia sanamu yake. Walikuwa mashahidi halisi, wa kweli wa Mungu.

⁷⁸ Kisha kuna wakati mwingine adhabu inapoendana na shahidi. Wakati mwingine, unapomshuhudia Mungu, inakubidi kuteseka kidogo.

⁷⁹ Unakumbuka wakati mama alipokwambia kuwa huwezi kukaa nyumbani, mradi tu unasoma Biblia na kupiga makelele? Au, baadhi ya majirani walisema, au watoto walisema, shuleni, “Ulikuwa mlokole,” au kitu fulani, kwa sababu ulikuwa shahidi wa kweli? Unakumbuka, kazini, jinsi watu wote walivyokucheka kwa sababu ulikuwa shahidi halisi? Unaoona? Jinsi huko mitaani ulifanyiwa mzaha, ulipotoa ushuhuda? Lakini hiyo ni ishara ya kweli ya shahidi halisi, wa kweli. Mungu anataka mashahidi.

Sasa baadhi ya watu wanasema, “Ninashuhudia kanisani.” Hilo ni zuri.

⁸⁰ Lakini, ndugu, acha Nuru yako iangaze mahali penye giza, mahali inapohitajika kweli, huko nje vichochoroni na barabara kuu, katika baa, huko nje, huko chini mtaani. Kila mahali ulipo, acha Nuru yako iangaze kama shahidi. Amina.

Angalia, ndipo jaribu kali linakuja.

⁸¹ Na kila mtu ambaye atamshuhudia Mungu itabidi apitie kwenye majaribu makali. Je, si ni ajabu jinsi Mungu anavyowaongoza watu Wake? Ajabu sana.

⁸² Mara tu Yesu alipobatizwa, alienda nyikani, akajaribiwe na ibilisi.

⁸³ Mara tu Israeli walipotoka, chini ya damu, wakatahiriwa, Roho Mtakatifu akiwaongoza katika mfano wa Nu—Nuru, moja kwa moja hadi Bahari ya Shamu. Na huko, wamesukumwa pembeni, milima upande mmoja, jangwa upande mwingine; huko Jeshi la Farao linakuja, na Bahari ya Shamu ikiwakatilia mbali. Mungu aliwaongoza moja kwa moja hadi mahali hapo. Kwa nini? Ili kujipatia utukufu. Ndipo Musa akaomba; naye Mungu akamwambia ashuke moja kwa moja kuelekea Bahari ya Shamu, akiwa ameishikilia fimbo yake mbele yake. Naye alipokuwa akitembea, Bahari ya Shamu ikasogea kutoka upande mmoja hadi mwingine, moja kwa moja wakavuka Bahari ya Shamu. Kwa nini? Njia ya Mungu iliwaongoza kupitia hapo.

⁸⁴ Mara tu walipotoka pale, moja kwa moja wakaingia kwenye Jangwa la Sini. Ajabu. Njia ya Mungu iliwaongoza moja kwa moja katika jaribu hilo kuu pale, walipomnung'unikia Mungu.

Walitoka hapo, na kuendelea, kutoka kwa mnung'unisti mmoja hadi mwingine, kutoka jaribu moja hadi lingine.

⁸⁵ Kama vile wimbo wa kale usemavyo, “Wengine kupitia majini, wengine kupitia mafuriko, wengine kupitia majaribu mazito, lakini wote kupitia kwa Damu.” Hiyo ndiyo njia ya Mungu ya kuongoza, kuongoza shuhuda zake, mashahidi Wake.

⁸⁶ Sasa, wakati ulipofika, majaribu, ya moto. Shadraka, Meshaki, na Abednego wakasema, “Mungu wetu anaweza kutuokoa na tanuru ya moto; lakini hata hivyo, asipotuokoa, hatutasujudu, tutakufa tukiwa shahidi halisi.”

⁸⁷ Ninapenda hilo. Ninapenda ujasiri huo wa kale. Kama vile mzee Buddy Robinson, alisema, “Bwana, nipe uti wa mgongo kama msumeno wa gogo.” Huyo ndiye aina ya shahidi wa kuigwa. Ujasiri! Mungu anapenda tuwe jasiri.

⁸⁸ Alimwambia Yoshua, kabla hajavuka, akasema, “Uwe hodari sana, kwa kuwa Bwana, Mungu wako, yu pamoja nawe kila uendako.”

⁸⁹ Unasema, “Vema, kama Mungu angeniambia kama alivyomwambia Yoshua, ningekuwa na ujasiri, pia.”

⁹⁰ Amemwambia kila mwaminio jambo lile lile. “Nitakuwa pamoja nawe, sikuzote, hata ukamilifu wa dahari. Sitakuacha wala sitakupungukia.” Jasiri! Haya twendeni tukaichukue ile ahadi basi. Mungu alitupa ahadi. Hebu tuwe shahidi wa kweli.

⁹¹ Kwa hiyo wakaiwasha ile tanuru, ikawa moto mara saba kuliko ilivyokuwa hapo awali.

⁹² Hivyo ndivyo ibilisi afanyavyo. Na, ndugu, hafanyi kitu nusu nusu. Anasukuma kila kitu alichu nacho, moja kwa moja ndani yako. Lakini, Mungu na ashukuriwe, Mungu ana kusukuma nyuma fulani anakosukuma Mwenyewe. Hiyo ni kweli. Vema. Mwangalieni. Kwa hiyo akasema . . .

⁹³ Sasa angalieni. Ninaweza kumwona Mfalme Nebukadreza akijiandaa kando ya ile tanuru kubwa, na moshi, na anga zilikuwa nyekundu.

⁹⁴ Nawazia, usiku kucha kulikuwa na mkutano wa maombi ukiendelea. Unajua, ikiwa unakuja kwenye jaribio . . .

⁹⁵ Hili hapa. Hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi; unategemea hisia na uwezo wako mwenyewe, badala ya kulipeleka kwa Bwana katika maombi. Hiyo ni kweli. Siku hizi tunaanza kumtuma mtu fulani mahali fulani, vema, unasema, tunashuka na kuwa na mashauri kidogo, na kukutana na kusema, “Tunapaswa kufanya *hivi*, au kwenda *hapa*, au kufanya *vile*.”

⁹⁶ Lakini Biblia, katika zile siku kabla hawajawatuma mitume, walikusanyika pamoja na kufunga na kuomba. Ndipo Roho Mtakatifu akasema, “Nitengeeni Paulo na Barnaba.” Roho

Mtakatifu! Mnaona, si maoni ya mwanadamu; bali Roho Mtakatifu akiongoza, akiongoza. Amina. Tazama.

⁹⁷ Sasa, mkutano wa maombi, usiku kucha, kwa hiyo iliwabidi waonyeshe walichoumbwa kwacho. Na, ndugu, kila mtu anayedai kuwa Mkristo, wakati mmoja ama mwingine huna budi kuonyesha umeumbwa kwa kitu gani. Ibilisi atakupa changamoto.

⁹⁸ Wakati maskini Tommy Osborn, wengi wenu mnamfahamu, alipokuja, nilikuwa nimeketi barazani. Akasema, “Ndugu Branham, mimi. . .” akasema, “Nilikuwa kwenye ule mkutano. Nilimwona yule mwendawazimu akianguka kukingama miguu yako.” Kasema, “Nifanye nini?”

⁹⁹ Nikasema, “Sasa, Tommy, usidai chochote ambacho huwezi kuthibitisha. Ibilisi atakupa changamoto juu yake. Naam, atakupa, na atafanya hivyo mara moja.” Nikasema, “Ndipo ikiwa huwezi kulithibitisha, unajua kinachokuja. Itakuwa ni aibu. Kwa hivyo hakikisha kuwa unasema kweli, kabla ya kutoa tamshi lako.”

¹⁰⁰ Na hiyo ni kweli, pia, Mkristo. Uwe na hakika kwamba, chini moyoni mwako, Mungu amekutenga na mambo ya ulimwengu na kukufanya kiumbe kipya, ndipo uende ukawaambie watu wewe ni Mkristo. Mpaka hilo litakapotukia, kaa moja kwa moja madhabahuni na ufe mpaka umekufa kabisa. Vema. Kufa mpaka uwe umekufa kabisa mpaka hata huwezi. . . Vema, hiyo ni kweli, umekufa!

Mnajua, nafikiri, siku hizi, tunawazika watu wengi kupita kiasi walio hai.

¹⁰¹ Mnazika watu wakiisha kufa. Hiyo ni kweli? Naaam, bwana. Sikiliza, ndugu, mtu aliyekufa hatabishana nawe. Unaweza kumwambia chochote unachotaka, umwite majina ya kila namna, hatasema neno. Kwa nini? Amekufa.

¹⁰² Na mtu ambaye amekufa katika Kristo, unaweza kumpa pombe, unaweza kumpa *hiki, kile*, ama *kinginecho*, lakini amekufa. Naye amefichwa ndani ya Kristo, kwa njia ya Mungu, ametiwa muhuri na Roho Mtakatifu. Amina. Ndiyo hiyo. Sasa, basi, hawezi kufanya mambo hayo, kwa sababu ha—hawezi tu kufanya hivyo. Ni kinyume na asili yake. Anakuwa kiumbe kipya.

¹⁰³ Hebu mchukue nguruwe mzee na kumwosha, na kumsugua, na kuzipodoa kucha za vidole vyake vya miguu, na kumpa rangi ya mdomo, na kumvika, nailoni zote utakazo; mfungulie, ataenda moja kwa moja kwenye kugaagaa na kugaagaa. Kusugua hakufai kitu. Angali ana asili ya nguruwe.

¹⁰⁴ Na kisha mchukue mwana-kondoo na kumtia kwenye shimo la matope, atapiga kelele mpaka umtoe nje. Kwa nini? Yeye ni asili ya mwana-kondoo.

105 Sasa, njia pekee ya kumzuia nguruwe asiingie kwenye matope ni kuibadilisha asili yake. Hiyo ni kweli.

106 Hiyo ndiyo njia pekee ya kumfanya Mkristo. Asili yake ibadilishwe, kutoka mwenye dhambi kuwa mtakatifu. Unaona? Na kuna dawa moja tu, hiyo ni Roho Mtakatifu. Ndipo wewe ni shahidi. Amina.

107 Sasa angalieni. Nataka mlipate hili, vizuri. Mfalme Nebukadreza alifanya ta—tangazo kwamba watu hawa wanapaswa kuchomwa moto. Basi asubuhi hiyo wakaja, wamefungwa mikono yao. Kulikuwa na ubao mnene mpana wa kutembelea pale, njia ya kufikia juu ya ile tanuru, ile tanuru kubwa, ikiwa wazi. Walikuwa wakishuka kwenye tanuru. Nao wakaanza safari ya kifo. Akasema, “Sasa angalieni, mna nafasi sasa. Mkitaka kuichukua, sawa.”

108 Wakasema, “Mungu wetu anaweza kutukomboza, lakini hatutaichukua.” Walikuwa mashahidi halisi, wa kweli, hadi mwisho.

109 Wakaanza kutembea kwenye hiyo njia, wakipanda, askari wakiwasukuma. Lile joto kali likawa baya sana hata karibu liwakabe roho hao askari. Ndipo alipokuwa tayari kuwasukuma kwenye hiyo tanuru ya moto, ninaweza kumsikia Shadraka akisema, “Aisee, mna hakika mliomba vya kutosha?”

“Naam. Ninaamini yote ni sawa sasa.” Sawa.

110 Halafu basi hata askari waliuawa, wale waliowaingiza. Na wakawasukuma. Hatua chache tu, nao wangewasukuma kwenye tanuru ya moto.

111 Sasa, wakati wote kukiwa na jambo linaloendelea duniani, kuna jambo fulani linaloendelea Mbinguni, pia. Nina picha mbaya hapa, inayozingatiwa sasa, ya mwaminio akielekea kwenye kifo chake. Lakini hebu tugeuze kamera yetu, usiku wa leo, kuelekea Mbinguni. Na wakati mambo yanapoendelea hapa chini, kuna jambo fulani linaloendelea Huko juu. Ninaweza kumwona Mungu, Mwana wa Mungu ameketi mkono wa kuume, akitazama chini.

112 Ninaweza kumsikia Malaika akija na kusema, “Bwana, mimi ni Gabrieli,” akiwa na upanga wake mkubwa mkononi mwake, akisema, “sasa, mimi, tangu siku ile uliponiumba, nimesimama upande Wako wa kuume. Nimefanya yale tu uliyoniambia nifanye. Je, umewaangalia hao mashahidi, asubuhi ya leo? Wanapanga kuwateketeza mashahidi watatu.”

Ninaweza kumsikia akisema, “Nimewaangalia usiku kucha.”

113 “Naomba nishuke huko chini.” Akasema, “Nitaondoa... Nitaibadilisha hiyo picha.” Naamini angeweza kufanya hivyo.

114 Lakini akasema, “Gabrieli, rudisha tu upanga wako kwenye ala yake. Siwezi kukuacha uende.”

115 Ndipo ninatazama akija hapa, upande Wake wa kushoto, huyu hapa anakuja Malaika mkuu, mwenye nguvu, jina lake Pakanga. Ana mamlaka juu ya maji. Naye anaanguka mbele Yake na kusujudu, na kusema: “Bwana, umewaangalia wale mashahidi? Mbona wao wanajitayarisha kuwateketeza asubuhi ya leo, kwa maana wanamshuhudia Mungu.”

Kasema, “Naam, nimewaangalia.”

116 “Naomba nishuke chini. Nitaifagilia mbali Babeli kutoka kwenye uso wa nchi.” Naamini angeweza kufanya hivyo. Akasema, “Ulinipa funguo. Na wakati wa mage-...au ulimwengu ulioitangulia ile gharika, nami nikakifurikisha kitu hicho chote, na kukifagilia mbali. Nitaifanya jambo lile lile, asubuhi ya leo, kama utaninii tu—utanipa tu upepo.”

117 Ninaweza kumsikia akisema, “Naam, Pakanga, hiyo ni kweli, unaweza kulifanya. Ni—ninajua unaweza kulifanya, lakini siwezi kukuacha uende.”

“Kwa nini, Bwana?”

118 “Simama hapa upande Wangu wa kushoto, maana siwezi kukuacha uende. Ninaenda, Mwenyewe. Nimewatazama, usiku kucha. Ninawatazama mashahidi Wangu. Ninaliangalia Neno Langu, pia, ili kulitimiza. Siwezi kukuacha uende. Kwa sababu, Ninaenda, Mwenyewe.”

119 Wako karibu hatua moja tu sasa, kuingia kwenye tanuru ya moto.

120 Je, si ni ajabu? Mungu hukuacha uje moja kwa moja kufikia hatua ya mwisho ya barabara. Inaonekana kana kwamba hajali; aliketii tu. Lakini Yeye anakuangalia. Ninawazia alipokuwa akitazama chini Babeli. “Jicho lake liko kwenye shomoro, nami ninajua Yeye ananitazama.” Anakutazama. Angalia.

121 Ndipo ninaweza kumwona anapoinuka kutoka kwenye Kiti Chake kikuu cha Enzi. Nguo Zake za ukuhani zinamshukia. Naye akatazama huko nje, na radi kubwa sana ilikuwa imeketi nyuma upande wa kaskazini. Ninaweza kumsikia akisema, “Njoo hapa, upepo wa mashariki, upepo wa magharibi, kaskazini na kusini. Ninataka kukuendesha, asubuhi ya leo.” Wakaingia chini ya radi hiyo na kufingirika karibu na—na Kiti cha Enzi. Naye akaweka miguu Yake juu ya radi hii kubwa, akanyosha mkono na kushika radi ya zizizaga na kupasua nayo anga, namna *hiyo*.

122 Na yapata mara ya kwanza walipochukua hatua hiyo ya mwisho, kuingia mle. Alishuka kando ya Mti wa Uzima, ama Mkondo wa Uzima, na kuokota mtende mkubwa wa kupepea. Ndipo walipoingia kwenye ile tanuru ya moto, kulikuwa na Mmoja kama Mwana wa Mungu amesimama katikati yao; akipepea upepo wote mwanana, mbali nao, na kwa kuwa wanaungua kwa muda mrefu. Mashahidi halisi, wa kweli!

Mungu atasimama na shahidi wa kweli. Hiyo ni kweli.

¹²³ Basi, angalia, wakati joto lote lilikuwa linawaka, na moto ulikuwa unawaka, moyo wa mfalme huyo ulifadhaika. Akasema, “Nendeni, mkaifungue ile tanuru, labda, muone kama kuna majivu yoyote yaliyosalia.” Nao walipoufungua mlango kwa nguvu, aliruka, akasema, “Mliwaweka wangapi mle ndani?”

Kasema, “Watatu.”

¹²⁴ Akasema, “Naona wanne. Na yule mwingine anafanana na Mwana wa Mungu.” Akisimama karibu na shahidi Wake.

¹²⁵ Mungu daima atasimama karibu na shahidi Wake. Amina. Mnajua huo ndio ukweli. Mungu ataleta tofauti, naye atasimama pamoja na wale wanaomshuhudia.

¹²⁶ Wakati mmoja kulikuwako na jamaa mdogo jina lake Daudi. Akatoka nje, kuwapelekea ndugu zake zabibu kavu, wakati mmoja, waliokuwa vitani. Basi baba yake, Yese, akamtuma huko. Sauli alikuwa ndiye mfalme. Wafilisti walikuwa upande mmoja na Waisraeli upande huo mwingine; handaki kati yao, na kijito cha maji kinapita.

¹²⁷ Na kama ibilisi afanyavyo daima, anapofikiri kwamba anaweza kushinda, ndugu, yeye husukuma kwelikweli.

¹²⁸ Kwa hiyo alikuwa na jamaa mkubwa mno pale, mwenye urefu wa kama futi saba ama futi nane, labda zaidi kidogo, labda futi kumi; mabega makubwa mno kama mlango wa ghala; mkuki mkubwa na silaha. Naye akasimama huko nje. Akasema, “Sasa nawaambia tunachopaswa kufanya. Mimi ndimi shahidi hapa, kwa Wafilisti. Hebu tumpate shahidi kutoka huko. Hebu majeshi yasipigane, bali tutoke tupigane. Na kama nikimwua, basi ninyi nyote mnatumikia; kama ataniua, basi tutawatumikia.”

¹²⁹ Mnaona jinsi ibilisi afanyavyo? Anapofikiri kwamba anaweza kushinda, anajivuna, anajisifu, na kupiga makelele.

¹³⁰ Sauli, futi saba, yeye mwenyewe, aliogopa kwenda kukabiliana naye. Ndipo majeshi ya Israeli yakashindwa, yakisimama nyuma vilimani, yakitazama ng’ambo.

¹³¹ Baada ya kitambo kidogo, huyu hapa maskini mvulana mmoja anakuja, akitembea pale. Maskini jamaa mwekundu; sio mkubwa sana; jamaa mdogo, aliyekonda, mwembamba. Lakini kulikuwa na kitu fulani kikipigapiga chini ya koti hilo dogo la ngozi ya kondoo, ambacho hao wengine hawakuwa nacho. Alipanda pale na kuwapa ndugu zake zabibu kavu naye alikuwa akizungumza nao kuhusu vita.

¹³² Baada ya muda kidogo, jitu hili kubwa lilitoka na kujisifu, kwa wakati usiofaa tu, kasema, “Nani atakuja na kupigana nasi?”

¹³³ Naye Daudi akasema, “Jamaa huyu ni nani?” Kasema, “Mnataka kuniambia, mtamruhusu Mfilisti huyo asiyetahiriwa

asimame hapo nje na kuyatukana majeshi ya Mungu aliye hai? Je, hatuwezi kuwa na mtu wa kusimama pale na kuzishuhudia nguvu za Mungu!” Wote waliogopa. Akasema, “Nitakwenda.” Napenda ujasiri huo. “Nitakwenda. Acheni nipigane naye.”

¹³⁴ Mbona, akapanda juu. Wakampeleka kwa Sauli, naye Sauli akasema, “Naam, mtu huyo ni shujaa kutoka ninii yake... Mbona, amekuwa shujaa tangu ujana wake, nawe si kitu ila kijana.”

¹³⁵ “Tazama!” Haleluya! Ninalipenda papa hapa. Daudi akasema, “Tazama, mtumishi wako...” kwa Sauli. “Bwana aliniruhusu nimwue dubu, kwa kombeo hili. Aliniruhusu nitoe mwana-mbuzi kutoka katika kinywa cha simba na kumwua. Nilimnyakua kwa masharubu nikamtoa kwake. Mimi ni shahidi.” Haleluya! Alikuwa mahali fulani. Alikuwa ameona kitu. Alikuwa amezijaribu Nguvu za Mungu, naye alikuwa shahidi.

¹³⁶ Hilo ndilo tunalohitaji leo, ni ujasiri zaidi. Hiyo ni sawa. Naam, bwana. Akasema, “Mimi ni shahidi wa yale ninayozungumzia.” Haleluya! Huyo ndiye Kanisa la Mungu aliye hai linamhitaji leo, ni shahidi ambaye amekuwa mahali fulani, ameona kitu fulani, naye anajua yale wanayozungumzia.

¹³⁷ Akasema, “Mimi ni shahidi wa Nguvu za Mungu. Dubu alipanda kwenda kumshika mwana-mbuzi, nami nikamwua.” Akasema, “Naye simba akakimbia na kumshika mwingine. Nikamshika kwa masharubu na nikamwua.” Akasema, “Basi Mungu aliyenisaidia kumwua dubu na simba, si zaidi sana atamtia Mfilisti huyu asiyetahiriwa mikononi mwangu?” Haleluya!

¹³⁸ Katika siku ambazo wanasema, “Siku za miujiza zimepita.” Wakati wanasema, “Dini ya zamani za kale haitatumika tena; hiyo ilikuwa kitu kwa babu na bibi.” Ndugu, nina furaha, usiku wa leo, ya kwamba kuna baadhi ya mashahidi wa dini ya mtindo wa kale ya Roho Mtakatifu ya anga za bluu, inayoua dhambi, ambayo inaua asili yenyewe na nguvu za Adamu za ibilisi, nao moyo wako unaweza kuwa safi. Haleluya! Loo! Shahidi! Kwa hiyo, loo, jamani!

Kasema, “Hawa watu wana kelele sana.”

¹³⁹ Mbona, wana jambo la kupigia kelele. Hakika. Sikilizeni, nitawathibitishia kwamba dini ya Biblia imekuwa na kelele sikuzote. Naam. Mungu alimwambia Ayubu, kasema, “Ulikuwa wapi wakati...” Ayubu aliwazia alikuwa mtu mkuu. “Ulikuwa wapi nilipouweka msingi wa dunia?”

¹⁴⁰ Mtu fulani, hivi majuzi, alisema, “Ndugu Billy, bado unahubiri baadhi ya aina hiyo mpya ya dini uliyo nayo?”

141 Nikasema, “La, bwana. Ninahubiri dini ya kale sana iliyowahi kuwako, na ile pekee iliyoko kweli, na iliyo na wokovu ndani yake.”

142 “Baadhi ya hizo, aina hiyo mpya,” kasema, “hatukuwa na hiyo hapa miaka michache iliyopita.”

Nikasema, “Hebu nikwambie, ndugu, ni ya kale kuliko ulimwengu ulivyo.”

143 Hiyo ni kweli. “Ayubu,” kasema, “ulikuwa wapi nilipoiweka misingi ya ulimwengu, hapo nyota za asubuhi zilipoimba pamoja na wana wa Mungu wakapiga kelele za shangwe?” Mamilioni ya miaka kabla ya kuwekwa msingi wa ulimwengu! Amina! Whiu! Hiyo ni kweli. Shahidi! [Ndugu Branham anapiga makofi mara moja.]

144 Mbona, wakati Haruni, kuhani mkuu, alipoingia Patakatifu pa patakatifu, huku amebeba damu, ilibidi wamvalishe kwa njia fulani, na ilimbidi atembeke kwa namna fulani. Ilibidi awe shahidi wa Mungu. Naye akaichukua ile damu na akaenda mbele. Na juu ya pindo za mavazi yake, chini, kulikuwa na kengele katika komamanga; kengele katika komamanga. Na ilibidi atembeke ili hiyo icheze, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana.” Nena kuhusu utakatifu! Na sababu ya hiyo kengele kulia dhidi ya komamanga, ndiyo njia pekee waliyojua ya kwamba Mungu hakuwa amemwua. Njia pekee ambayo alijua alikuwa hai, alipokuwa huko nyuma, wangeweza kusikiliza na kuisikia hiyo kengele, kusikia kelele.

145 Ndugu, nakwambia, tunahitaji makomamanga na kengele zipigwe pamoja, usiku wa leo, hivyo, kwa sauti ya shangwe kwa Bwana, kama shahidi. Mungu bado yu hai na anatawala! Amina! Kweli! Shahidi wa aina gani? Hao mashahidi kama wale waliopanda kwenye kile chumba cha juu, huko juu, na kupata ubatizo wa Roho Mtakatifu. Walikuwa wametengeneza komamanga na kengele, wakakusanyika pamoja. Waliyumbayumba kama walevi, chini ya nguvu za Roho Mtakatifu. Mungu angali anao mashahidi, nao ni kitu kile kile. “Mtakuwa mashahidi Wangu wa Nguvu hii, katika Yerusalemu, Uyahudi, na Samaria, na Jeffersonville, Indiana.” Amina! Haleluya! Angalieni!

146 Daudi akasema, “Mnataka kuniambia yule Mfilisti asiyetahiriwa,” vinginevyo, “asiye Mkristo, mtu yule asiye- . . .”

147 Tohara ni nini? Mtu huyo huko nje aliye na Roho Mtakatifu.

148 “Akiwa na D.D. zake zote, anaweza kusimama na kumtukana Mungu aliye hai?” Loo, jamani! “Anawezaje kufanya hivyo?” Kasema, “Yeye hajatahiriwa.”

149 Sasa tumetahiriwa na Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu ndiye tohara yetu. Kwani unataka kuniambia ya kwamba unawaacha hawa Madaktari wa Uungu, na Ph.D., na D.L.D.,

na D maradufu, wasimame huko nje na kutwambia kwamba “dini ya zamani za kale si sahihi”? Wakati, ubatizo wa Roho Mtakatifu unathibitisha ya kwamba ni wa kweli. Wasema, “Watu hawatakuja.” Naam, watakuja. Amina.

¹⁵⁰ Mzee Yohana Mbatizaji, alipoanza kuhubiri, alikuwa ndiye mhubiri mashuhuri kuliko wote wa wakati huo wote. Alikuwa mtu mnyenyekevu sana. Alienda nyikani akiwa na umri wa miaka tisa. Hakupata Ph.D. Lakini alifanya nini? Hakujitokeza na ukosi uliopinduliwa, au—au kujua *Wimbo Wa Kumsifu Mungu*, au *Kanuni ya Imani ya Mitume*. Lakini alikuwa shahidi wa Mungu. Alipotoka katika nyika ya Uyahudi, alihubiri Injili ya namna hii, akiwa amejizungushia maskini ngozi ya kondoo, namna *hii*.

Loo, jamani! Lakini alitikisa mikoa yote ya kandokando ya Yerusalemu, na Uyahudi, na kando ya Yordani. Kwa nini? Alimhubiri Kristo; si katika jambo la kihistoria, lakini katika tukio la sasa, ukweli wa sasa. Haleluya!

¹⁵¹ Leo tunahubiri historia, duniani kote, na ufufuo wa Kristo. Lakini vipi kuhusu wewe kama mtu binafsi, moyoni mwako, je, amefufuka katika Maisha mapya? Je, maisha ya kale yamekufa?

¹⁵² Daudi akasema, “Mtamwacha huyo Mfilisti asiyetahiriwa asimame hapo na kusema mambo kama hayo? Mbona,” akasema, “Nitakwenda kupigana naye.”

¹⁵³ Kwa hiyo, muda si muda mnajua, Sauli akasema, “Naam, ikiwa umedhamiria kwenda, nitakupa silaha ya—yangu. Nitakupa ngao yangu, chapeo yangu na upanga wangu.” Loo, jamani!

¹⁵⁴ Sikilizeni. Wakati kijana Daudi alipopata kitu hicho kikubwa sana. . . Hebu wazia, mabega madogo namna *hiyo*; na hayo mabega kwenye ngao hiyo, kubwa namna *hiyo*, ya hiyo dirii. Wakamvisha, maskini jamaa huyo asingeweza kutembea.

¹⁵⁵ Sikilizeni. Tuligundua kwamba ngao ya kikanisa haitamwenea mtu wa Mungu. Hiyo ni kweli. Theolojia yako yote haitalingana na Nguvu za Mungu. Huhitaji theolojia. Huhitaji elimu. Unachohitaji ni moyo uliojisalimisha, kwa Neno la Mungu, kuwa shahidi wa kweli.

¹⁵⁶ Haingemfaa mtu wa Mungu. Akasema, “Niondoleeni kitu hiki. Sihitaji Ph.D yako.” Amina! Kasema, “Mimi ni shahidi!” Wa nini? Kasema, “Sijawahi kujaribu vitu vya aina hii. Sijui chochote kuhusu theolojia yako. Niache niende, jinsi Bwana alivyoniokoa na simba na dubu.”

¹⁵⁷ Ndivyo ninavyosema leo, ndugu. “Usiniache niende na saikolojia, bali niache niende na ubatizo wa mtindo wa kale wa Roho Mtakatifu ambao ulinitoa katika kinywa cha Baptisti na kunikomboa. Acha niende hivyo.”

158 “Loo,” alisema, “siwezi kwenda na haya yote sijawahi kuyajaribu. Sijui chochote kuyahusu. Nitajuaje jinsi ya kusimama na kurudia kanuni hizi zote za imani na kila kitu kama hicho? Sijui chochote kuihusu.” Kasema, “Niondolee kitu hiki.”

159 Kwa hivyo waliiondoa. Akajisikia vizuri sana. Akarudi nyuma na kuchukua kombeo lake dogo. Alijisisikia kukimbia. Unajua jinsi unavyojisikia unaposhika kombeo lako mkononi mwako. Akatazama kule.

Naye Goliathi akasema, “Utafanya nini kuhusu hilo?”

160 Daudi akasema, “Naja mimi.” Amina. Akachukua kombeo lake dogo, akatelemka mbio akavuka kijito na kuokota mawe matano. Akaweka moja mle ndani, akalizungusha mikononi mwake.

161 Naye Goliathi akasema, “Mnataka kuniambia ya kwamba maskini mtakatifu huyo anayejifingirisha, ama, mnajua, jamaa huyo mdogo asiye na eli-... au chochote alichu, akija pale kukutana nami?” Akasema, “Mimi, pamoja na digrii zangu zote na kadhalika, mbona, hata siwezi kutumia wakati wangu pamoja naye. Akizungumza juu ya uponyaji wa Kiungu, akizungumza juu ya Nguvu za Mungu, akizungumza juu ya wokovu; siwezi hata kuutumia wakati wangu pamoja naye.” Lakini alikuwa shahidi wa kile alichokuwa anazungumzia.

162 Iwapo mwanamume au mwanamke ni shahidi wa kile wanachozungumzia, usijali, itawabidi watumie muda, maana msimu wa kuua nguruwe utakuwa umewadia, ndugu, mbao za kukwaruza zitatolewa. Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Vema.

163 Akaweka maskini jiwe hilo dogo chini kwenye kombeo hilo. Huyu hapa akaenda, kuvuka tawi na kupanda juu ya kilima, akikimbia kukutana na huyu.

164 “Mbona,” alisema, “tazama!” Akasema, “Unakutana nami kama...” Akasema, “Vema, wewe, nitakunyanyua kwenye ncha ya mkuki wangu,” pengine urefu wa futi thelathini au arobaini. Kasema, “Nitakunyanyua huko na nitawapa ndege nyama yako, wale, leo.”

165 Mwangalie Daudi, shahidi sasa. Alijua alichokuwa anazungumzia. Upinzani ulikuwa dhidi yake. Hakika, ulikuwa dhidi yake. Lakini alijua alikuwa... Alikuwa shahidi. Alijua alichokuwa anazungumzia.

166 Hivyo akasema, “Unakutana nami kama Mfilisti, katika jina la Mfilisti, ukiwa na silaha na mkuki. Lakini nitakutana nawe katika Jina la Bwana, Mungu wa Israeli.” Amina. Hiyo ndiyo tofauti. Hilo ndilo lililoleta tofauti. Naye akasema “leo” angeweza “kuua.”

Mbona, hilo jitu likamcheka, nalo likaenda kumwua.

167 Maskini Daudi anaanza. Wakati alipofikia umbali wa kurushia kombeo, alikuwa...Tazama, alikuwa na mawe matano, J-e-s-u-s, yakiwa yamefungiwa kwenye vidole vitano, i-m-a-n-i. Ndugu, alikifanya hicho kitu kufanya kazi vizuri, kikazunguka na kuzunguka na kuzunguka.

168 Nawe unapopata imani katika Yesu Kristo, akifanya kazi kwa mwendo wa kudumu katika nafsi yako, jambo fulani litatukia. Dhambi na magonjwa yatakuondokea; ibilisi watatawanyika kama mende sakafuni wakati wa kiangazi, taa inapowashwa.

169 Huyu hapa anakuja, i-m-a-n-i katika Yesu. Huyu hapa anakuja, "Ninakutana nawe katika Jina la Bwana Mungu wa Israeli," kisha akaanza kulizungusha hilo kombeo, Roho Mtakatifu akalirusha jiwe hilo moja kwa moja hadi kwa Mfilisti huyo na kumwua. Daudi akautwaa upanga wake mwenyewe, akakikata kichwa chake, akakiinua, akasema, "Hima, wavulana!" Kasema, "Huyu hapa. Niliwaambia Mungu angelitenda." Haleluya!

170 Alikuwa shahidi. Alijua alichokuwa akizungumzia. Alikuwa amekijaribu. Alikuwa amekithibitisha. Hakujua chochote kuhusu silaha na mkuki, lakini alijua kile alichokuwa nacho mkononi mwake. Mungu alikuwa pamoja naye.

171 Sijui, hatujui, kuhusu mawazo yenu makubwa na mambo kama hayo. Lakini tunajua Roho Mtakatifu ni nini, na tunajua anachotufanyia, kwa hiyo tunataka kuwa shahidi. Sasa huna budi kwenda kumpokea, kwanza, kabla ya kuweza kuwa shahidi.

172 Kulikuwa na jamaa, wakati mmoja, jina lake Eliya. Mungu alikuwa pamoja naye. Alikuwa amemwona Mungu, katika majaribu makubwa, alikuwa amemwona Mungu akitenda mambo. Kwa hiyo akaona dhambi ikija juu ya taifa, kwa hiyo akasema, "Sasa hebu kidogo."

173 Akapanda kule juu na kuomba, naye Mungu akampa shahidi. Akasema, "Sasa wewe shuka ukamwambie mfalme kwamba hata umande hautaanguka isipokuwa mimi... isipokuwa uagize."

174 Anashuka na kumwambia mfalme hivyo. Akapanda kule, akaketi chini. Yeye...na hapo...

175 Basi ungeweza kuwazia? Ninaweza kusikia baadhi ya watu wakisema, "Mzee huyo amerukwa na akili. Mnaona? Mbona, anasema hakutakuwa na mvua mpaka aiagize."

176 Lakini alikuwa shahidi wa Mungu. (Mnaona?) Alijua alichokuwa akizungumzia. Alijua yale Mungu angefanya, maana Mungu daima hutimiza Neno Lake. Naye Eliya alijua hilo. Kwa hiyo, alijua kwamba Mungu alikuwa amemwambia

mvua haitanyesha, kwa hiyo akaenda na kuwaambia kuwa haitanyesha.

¹⁷⁷ Kama Mungu alisema, kama unaweza kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, basi nenda ukaupokee. Mungu anaposema uponyaji ni kwa ajili yako, basi nenda ukaupokee. Kama wewe ni shahidi, endelea, shuhudia kwa ajili Yake. Mungu aliahidi jambo hilo; hawezi kusema uwongo. Haijalishi wanasema nini, “Siku za miujiza zimepita,” hilo, acha tu hilo liende. Ni Neno la Mungu tunalochukua, si la mtu mwingine.

¹⁷⁸ Ninaweza kuona, muda si muda mwajua, huyu hapa mzee Eliya anakuja, akaenda kule.

¹⁷⁹ Naye akasema, “Angalia mwendawazimu yule sasa! Amepanda, kilele cha kilima kule, na kuketi karibu na kile kijito, Kerithi. Ni tamasha ya kusikitisha jinsi gani, mzee yule kule juu; ndevu ndefu za kijivu. Naye ana yapata umri wa miaka sabini, na fimbo mkononi mwake. Chupa ndogo ya mafuta; mbona, atakufa njaa, kule juu.”

¹⁸⁰ Lakini, baada ya kitambo kidogo, ukame ukaja, na kuanza kuendelea. Nawe unajua, hao watu kule chini, waliofikiri ya kwamba alikuwa mwendawazimu, ikatokea waliona kwamba huko juu alikuwa akila milo mitatu kwa siku, akiwa na wakati mzuri. Naam. Alikuwa na maisha bora zaidi kuliko watu wengi hapa usiku wa leo. Alikuwa na baadhi ya wapagazi. Hiyo ni kweli. Wapagazi wakapitia pale, kunguru wakapitia pale kila siku, na kumletea sambusa, wakampa kwa ajili ya kifungua kinywa chake.

¹⁸¹ Jamaa fulani alisema, si muda mrefu uliopita, alisema, “Mhubiri, unamaanisha unaamini hayo?”

Nikasema, “Naam, bwana.”

Akasema, “Unataka kuniambia kwamba unaamini kwamba alikula?”

Nikasema, “Naam, alikula.”

“Ni vipi wewe. . . Angepata wapi samaki?”

Nikasema, “Sijui.”

“Angepata wapi mkate?”

Nikasema, “Sijui.”

Kasema, “Unafikiri alienda kwenye tanuru ya mikate?”

¹⁸² Nikasema, “Siwezi kukwambia. Lakini, jambo pekee ninalojua, kunguru waliileta. Alikila, akashukuru kwa ajili yake, na kufanya yale ambayo Mungu alimwambia afanye.”

¹⁸³ Hiyo ni sawasawa na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Unasema, “Ni kitu gani kinachowafanya watu hao kupaza sauti?” Sijui. “Una maana gani?” Ni Mana inayotoka kwa Mungu, kutoka Mbinguni. “Unamaanisha kweli unahisi jambo fulani kweli? Siamini.” Vema, si lazima. Roho Mtakatifu huileta. Ninaila tu,

na kushiba, na kupaza sauti na kuwa na wakati mzuri. Acha ulimwengu uende na uamini kile wanachotaka. Roho Mtakatifu! “Lakini Yeye anaipata wapi? Hiyo Mana inatoka wapi? Kitu chochote kinatoka wapi angani, ambacho huwezi kuona?” Sijui, lakini kinafika hapa. Amina.

¹⁸⁴ Je, wewe ni shahidi Wake? Je, umeonja, Bwana ni mwema? Je, unajua unachozungumzia? Ubatizo huo wa Roho Mtakatifu ni halisi tu, usiku wa leo, kama maisha yako yalivyo, Nguvu za Mungu ziletazo wokovu. Hakika, ni mzuri.

¹⁸⁵ Yeye aliketi hapo na kula. Alipokuwa tayari kunywa, alienda tu kando ya kijito na kunywa, hivyo tu. Nao walidhani alikuwa na kichaa. Hapana. Alikuwa shahidi wa Mungu. Hiyo ni kweli.

¹⁸⁶ Na muda si muda wajua, kile kijito kilipokauka, Yeye alisema, “Sasa nimetayarisha mjane wa kukutunza.” Jamani, ni mahali jinsi gani kwa mhubiri kwenda, kwenye nyumba ya mjane! Lakini Mungu alisema, “Ni—nilipatarisha.” Kwa hiyo anashuka huko. Alikuwa awe shahidi kule chini. Hivyo mjane huyu . . .

¹⁸⁷ Kwa hiyo anashuka kwenda kule, naye alikuwa akitembea barabarani. Kulingana na lile ono, alipaswa kumwona mwanamke barazani, nadhani. Akamwona mwanamke barazani, akasema, “Huyo ndiye, kwa hivyo nitapita tu pale.”

¹⁸⁸ Akasema, “Nenda, uniletee maji kidogo ya kunywa, na ki—kipande cha unga, au—au keki,” hasa, “mkononi mwako.”

¹⁸⁹ Akasema, “Kama Bwana aishivyo, na nafsi yako haifi kamwe,” kasema, “Nina unga wa kutosha tu kwenye pipa, na mafuta ya kutosha katika chupa, kuoka keki moja ndogo. Nami niko hapa nikioka . . . nikiokota vijiti viwili. Na,” kasema, “nami nitajipikia keki nafsi yangu na mwanangu. Na, mara tu tukiula huo, tukafe.”

Akasema, “Nenda, uniletee keki moja kwanza.” Amina.

¹⁹⁰ “Utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu.” Je, umewahi kushuhudia kwamba hiyo ni kweli? Mtangulize Mungu. Toa zaka zako, kwanza. Lipa kila kitu, kwanza. Mlipe Mungu. Omba kwanza, asubuhi. Omba, siku nzima. Mpe Mungu nafasi ya kwanza katika kila jambo. Utakuwa shahidi.

Anakimbia ndani moja kwa moja. Alikuwa na vijiti viwili.

¹⁹¹ Katika njia ya kale ya kimashariki, walitumia vijiti viwili. Ilikuwa ni vijiti viwili, vilivyokingamana, *hivi*, na moto ulikuwa katikati. Wahindi bado wanaitumia, nao husogeza magogo mbele yanapoungua. Huo ulikuwa ni msalaba, Kristo, ambapo moto ulikuwa katikati.

¹⁹² Walichukua sadaka kidogo ya unga, wakaweka unga huo uliosagwa, wote umesagwa vile vile tu, “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Alimiminia mafuta ndani, ambayo yalikuwa ni Roho Mtakatifu. Na kuyachanganya pamoja, Roho

Mtakatifu na Kristo; anaenda kutengeneza keki nyembamba sasa, ndugu! Amina. Loo! [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Usifikiri mimi nina wazimu. Ninasikia tu kubarikiwa, usiku wa leo. Sawa.

Angalieni, “Niokee keki ndogo, kwanza.”

¹⁹³ Kwa hiyo akatwaa sadaka ya unga, Kristo, akamwaga Roho Mtakatifu ndani yake, na kuichanganya, na kuiweka juu ya msalaba na kuipika. Loo, ndugu, nena kuhusu keki, hiyo ilikuwa moja yazo!

¹⁹⁴ Akatoka nje, akaleta ile keki nyembamba, na tone la mwisho la maji aliyokuwa nayo. Naye nabii akasimama pale na kuila, kisha akanywa hayo maji. Kasema, “Sasa rudi ukatengeneze moja kwa ajili yako na mwanao. Kwa kuwa, BWANA ASEMA HIVI, lile pipa halitapunguka, wala chupa haitaisha, hata siku ile Mungu atakapoleta mvua juu ya nchi.”

¹⁹⁵ Nini? Shahidi. Hiyo ni kweli. Mjane huyo alikuwa shahidi nchini.

¹⁹⁶ Baada ya nabii huyo mkuu kuchukuliwa, na Eliya akachukuliwa; mahali pake, Elisha alipachukua mahali pa Eliya.

¹⁹⁷ Loo, naweza kuwazia shahidi wa aina hii. Siku moja, alianza kuondoka, naye akamwona Eliya. Akatupa vazi lake juu yake, akambariki, naye akamchinja maksai na kutoa dhabihu, akionyesha ya kwamba mambo yote ya ulimwengu yalikuwa yamekufa, nyuma yake.

¹⁹⁸ Hiyo ndiyo njia ya kumjia Mungu. Ua kila kitu nyuma yako. Teketeza madaraja yote. Usiiweke hiyo chupa ili uipate kesho. Wala usikiweke kitu hiki kingine ili ukipate kesho. Kiondoe kitu hicho; kichome moto. Amina. Kuwa shahidi halisi. Toka nje, ndugu, bila viatu. Hiyo ndio njia. Samahani kwa matamshi hayo, lakini hiyo ndiyo njia pekee niijuayo jinsi ya kusema. Vema, kwa hivyo sasa wewe—wewe. . . Mambo yanaenda kutokea hapa. Vema. Angalia.

¹⁹⁹ Ndipo akaanzia Gilgali, akaenda mpaka kwenye shule ya manabii. Nami nataka mwone, alipofika kule kwenye shule ya manabii, alisema, “Bwana ananiongoza kwenda Yordani.”

²⁰⁰ Hatua tatu ambazo Elisha alimfuata Eliya. Naye Eliya alikuwa mfano wa Kristo; Eliya. Elisha, mfano wa Kanisa. “Ninapanda kwenda Gilgali,” kwanza, kuhesabiwa haki kwa imani. Na kisha akasema, “Sasa wewe kaa hapa,” kwa Kanisa. Eliya, Elisha; kwa Eliya. . . Nabii kijana na mzee, mfano wa Kristo na Kanisa.

²⁰¹ Akasema, “Kama nafsi yako iishivyo, sitakaa hapa, lakini ninaenda pamoja nawe.”

202 Naye akapanda mpaka Gilgali. Naye alipofika huko, akasema, “Sasa wewe kaa hapa. Bwana ananiita kwenye shule ya manabii.”

203 Kwa hiyo akasema, “Kama Bwana aishivyo, na nafsi yako haifi kamwe, mimi ninaenda pamoja nawe. Sitakuacha.”

204 Hilo ndilo Kanisa. Mnaona? Weka macho yako kwa Yesu. Popote anaposogea, nenda. Kama akitoka katika kanisa la Methodisti, ambatana Naye moja kwa moja. Akitoka kwenye kanisa la Baptisti, ambatana moja kwa moja Naye. Akitoka kwenye Maskani ya Branham, ambatana Naye moja kwa moja. “Sitakuacha! Haidhuru mama alikuwa mfuasi wapi, baba alikuwa mfuasi wapi, ambako *hili* lilitokea, ama lingine; nitaenda pamoja na Wewe. Sitakuacha!” Haleluya! “Mimi ni shahidi Wako. Siwezi kwenda; Wewe ni sehemu yangu.”

205 “Njoo, nami nitafuata.” Naye anaenda kwenye shule ya manabii.

Kisha akasema, “Wewe kaa hapa.”

206 Ndipo baadhi ya manabii wakamwambia Elisha, akasema, “Je, unajua bwana wako ataondolewa kwako?”

207 Akasema, “Najua. Lakini nyamazeni.” Amina. Napenda hilo. “Nitakaa moja kwa moja pamoja naye, haidhuru wengine wanasema nini.”

208 Naye Eliya akageuka na kusema, “Sasa wewe kaa hapa, kwa maana Mungu ananituma kwenda Yordani.”

209 Maeneo matatu. Kuhesabiwa haki, Gilgali; utakaso, shule ya nabii; na kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, huko Yordani, ambapo Yordani inawakilisha kifo. Angalieni! Martin Luther; John Wesley; Pentekoste, kushuka mpaka Yordani, wakati wa kufa.

210 Kwa hiyo, Eliya, alitembea moja kwa moja mpaka mtoni, pamoja na Elisha. Nao walipofika Yordani, kifo, hatua ya mwisho ya safari; nabii mzee akaunyosha mkono wake, akalivua vazi lake, akayapiga hayo maji, nayo hayo maji yakagawanyika huku na huku na hao wawili wakavuka, ilikuwa ni nchi kavu. Wahubiri walisimama kando, na kuwatazama wakivuka. Amina.

211 Walipofika upande wa pili, sasa, baadaye! Loo, natumaini hili litaingia kwenye Maskani ya Branham, moja kwa moja mpaka kwenye mafuta yaliyomo ndani ya mfupa. Si alipokuwa Gilgali; si alipokuwa kwenye shule ya nabii; wala alipokuwa ng’ambo hii ya Yordani; lakini baada ya kuvuka Yordani, wakimfuata kila hatua ya njia.

212 Uko tayari; unasema, “Ninamkubali Yesu kama Mwokozi wangu binafsi. Nitaziacha tabia zangu mbaya.” Lakini shuka mpaka Yordani, ambapo inakubidi ufe; ambapo mambo yote

ya ulimwengu, marafiki wako wote na kila kitu, wamekuacha. Weka jicho lako Kwake pekee.

213 Halafu nini? Akasema, “Nitaambatana nawe, moja kwa moja kupitia Yordani.” Amina. Naipenda hiyo. Kwa nini? “Nitakuwa shahidi wa hili,” naye akavuka Yordani.

214 Angalia. Hili hapa. Nawataka mlipate. Baada ya kuvuka Yordani, ndipo akasema, “Unataka nikufanyie nini?” Hilo ndilo Kristo anataka kujua kuhusu kanisa, usiku wa leo. “Baada ya kutengwa na mambo ya dunia, baada ya kufanyika kiumbe kipya katika Kristo Yesu, baada ya kuzaliwa mara ya pili, ukajazwa na Roho Mtakatifu, ukavuka Yordani, mambo yote ya ulimwengu yamekufa, nyuma yako; sasa omba nikutendee nini.” Napenda hili.

215 Akasema, “Kwamba sehemu maradufu ya Roho yako ije juu yangu.” Mhubiri huyo alijua alichokuwa anazungumzia. “Sehemu maradufu, maana ninataka kushuhudia kiasi hicho.”

216 Akasema, “Umeomba neno gumu. Lakini ukiniona nitakapoondolewa, utaipata. Ulichoomba utapata.” Sasa, ndugu, nena kuhusu mhubiri kumwangualia huyo mwingine; alikuwa amemkazia macho kweli!

217 Hivyo ndivyo Kanisa linapaswa kufanya usiku wa leo, kwa sehemu maradufu ya Roho, anamwangualia Kristo, akimwangualia Roho Mtakatifu, jinsi anavyosonga mbele. Angalieni.

218 Alisema, “Umeomba neno gumu.” Lakini asingeweza kuweka jicho moja juu ya ulimwengu na jicho moja kwa Eliya. Ilimbidi kuweka macho yote mawili moja kwa moja kwa Eliya, na kumfuata.

219 Shida yake ni, usiku wa leo, tuna Wakristo wengi sana, wanaodai kuwa Wakristo, huku jicho moja liko juu ya ulimwengu na hilo lingine msalabani. Utaanguka, bila shaka kabisa. Acha macho yako yawe pamoja, moyo wako uwe pamoja, mawazo yako yawe pamoja. Amina. Ndugu, hilo linasugua, lakini hilo linaumiza, lakini ni zuri.

220 Sisi, kama watoto wadogo, tulizoea kunywa mafuta ya mbarika, wakati wote. Mama, kule nyuma, alikuwa akinipa mafuta ya mbarika, nami ningeshikilia pua yangu na kuziba kinywa. Angesema, “Mpenzi, ikiwa ni . . .”

Ningesema, “Kitu hicho kinanichefua sana!”

221 Angesema, “Kisipokuchefua, hakikufai kitu.”

222 Kwa hiyo, labda, hilo hapo. Labda, Injili, je, inaweza kutumika kwa njia iyo hiyo? Isipokuchochea kabisa, haitakufaa kitu.

223 Weka macho yako juu ya Kristo. Zidi kusonga mbele. Usijali ulimwengu unasema nini. Zidi kusonga mbele. “Wale walio wana wa Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu.” Je, hiyo

ni kweli? “Sasa basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu, wasioenenda kwa kuufuata mwili, au mambo ya dunia, bali mambo ya Roho.” Hakuna hukumu; kuendelea kutembea. Sasa angalieni.

²²⁴ Na wakati alipokuwa akipandishwa juu, baada ya kitambo kidogo gari la Moto likashuka, likamchukua Eliya, naye akalipanda. Ndipo alipokuwa akipaa juu, akavua vazi lake, namna *hii*, akalitupa nyuma, nalo likaanguka chini, wakati farasi wa . . . na gari la Moto lilipomchukua.

²²⁵ Loo, nawatakeni mlipate hili sasa. Ni mfano mzuri jinsi gani! Elisha, yule nabii kijana basi, yule ambaye alikuwa shahidi wake, pamoja na nguvu zote alizokuwa ametumia. Mambo yote ambayo Eliya alifanya, Elisha alikuwa shahidi wake. Ndipo akaokota vazi lile lile, akalitupa juu ya mabega yake mwenyewe, akaanza kutembea kuelekea Yordani; mfano mzuri, mkamilifu. Akashuka mpaka Yordani, akavua lile vazi, akalishika mikononi mwake, na kuyapiga maji. Kasema, “Yuko wapi Mungu wa Eliya?” Nayo maji yakagawanyika, huku na huko. Mfano wa Kanisa linalomfuata Yesu, likizona nguvu Zake, likiona miujiza Yake.

²²⁶ Naye, siku moja, aliulizwa. Wengine walisema, hebu . . . Mwanamke mmoja alisema, “Acha mwanangu aketi mkono wa kulia na mmoja mkono wa kushoto.”

Akasema, “Mwaweza kunywea kikombe ninyweacho Mimi?”

Kasema, “Naam.”

“Je, mwaweza kubatizwa ubatizo nibatizwao Mimi?”

Kasema, “Naam.”

²²⁷ Kasema, “Kweli, mtaweza; lakini mkono wa kuume na mkono wa kushoto, si langu Mimi . . .” Kwa maneno mengine, “Ubatizo ule ule nilio nao, mtakuwa nao, pia.”

²²⁸ Basi Kanisa lilipomwangalia, alipoenda kwenye Pentekoste . . . Alikwenda chumba cha juu na akala chakula cha jioni. Akatoka kwenda Kalvari, akasulubiwa. Na ndipo wakati Kanisa, lililoitwa litoke, lilimwangalia, alipoondoka kwa kupaa Kwake, akitwaliwa juu. Akasema, “Sasa nitawatuma ninyi katika pande zote za ulimwengu, mkawe shahidi Kwangu. Lakini kabla hamjaenda, ngojeni huko juu katika mji wa Yerusalemu; maana, vazi lili hili la Roho Mtakatifu lililo juu Yangu, litashuka juu yenu. Nitalirudisha.”

²²⁹ Nao wakapanda mpaka mji wa Yerusalemu, haleluya, na kule wakabatizwa kwa Roho Mtakatifu yule yule aliyekuwa juu ya Yesu Kristo. Haleluya! “Ndipo ninyi ni mashahidi Wangu, kama vile Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

²³⁰ Naye Roho Mtakatifu yeye yule aliyekuwa juu ya nabii Elisha, Eliya, alikuwa juu ya Elisha maradufu. Na sisi, usiku wa

leo, kama kanisa la Mungu, ndugu, dada, ambao tumedai kubusu kingo za kikombe kilichobarikiwa cha baraka Yake, pamoja na ubatizo wa Roho Mtakatifu ukishuka juu yetu na kutufunika, ukitubatiza katika Roho Wake, nasi tukienda huko nje kama mashahidi Wake. Tunawezaje kunyamaza katika siku kama hii, wakati ufisadi na upuuzi uko kila upande! Hebu na tusimame na kushuhudia Ukweli. Amina. Ajabu! Loo, jamani!

²³¹ Sina budi kuacha. Ninajisikia kama ningeweza kuanza sasa hivi na kuhubiri, naamini. Ni—ninaanza tu kujisikia vizuri.

²³² Lile vazi, sehemu maradufu! Yesu alisema, “Mambo niyafanyayo ninyi nanyi mtayafanya, na makubwa zaidi,” mengi zaidi, sehemu maradufu. “Nyinyi ni mashahidi Wangu baada ya kupokea sehemu maradufu.” Hebu tumwangelie Yeye. Weka macho yako juu Yake. Vazi liko chini. Vazi liko hapa, usiku wa leo. Roho Mtakatifu yeye yule aliyekuwa juu ya Yesu Kristo yuko katika kanisa hili, usiku wa leo, kumvika mwaminio yeyote aliye humu ndani, kwa Nguvu zitokazo Juu. Ndipo mtakuwa mashahidi Wake katika Yerusalemu, Uyahudi, Samaria, Afrika Kusini, Asia, popote uendapo. “Yeye yule jana, leo, na hata milele.”

“Ngojeni!” Si ajabu Filipino angeweza kushuka na kuhubiri!

²³³ Si ajabu, walipompiga kwa mawe maskini yule jamaa, Stefano, naye akatazama juu Mbinguni; mawe yakimpiga pande zote mbili za kichwa, zikiuponda maskini ubongo wake ardhini. Alitazama juu na kusema, “Tazama, naona mbingu zimefunguka, na Yesu amesimama mkono wa kuume wa Mungu.” Alikuwa shahidi.

²³⁴ Si ajabu, Paulo, Sauli alipokuwa njiani kwenda kule, macho yake yalipofushwa wakati Nuru ilipomwangukia. Naye akasema, “Ni nani, Bwana, ambaye na—ambaye ninakutesa?”

²³⁵ Akasema, “Yesu.” Naye akasema, “Shuka kwenye njia iitwayo Nyofu.”

²³⁶ Naye alikuwa na mhubiri kule chini, ambaye aliona maono, kwa hiyo yeye. . . jina lake Anania. Naye Anania aliona ono la Paulo. Akaingia ndani akamwekea mikono, na kusema, “Ndugu Sauli, Bwana Yesu Yule aliyekutana nawe njiani, amenituma nikuwekee mikono yangu, upate kuona na kujazwa na Roho Mtakatifu, kwa maana alinionyeshwa kwamba huna budi kuwa shahidi mkuu Kwake.”

²³⁷ Shahidi! Kwanza, nini? “Upokee kuona kwako, na umpokee Roho Mtakatifu.” Magamba yakatoka machoni mwake. Akainuka na kushuka hadi Mto Dameski, akabatizwa. Nawazia walikuwa na wakati mzuri huko chini! Nanyi je?

²³⁸ Kulikuwako na Sauli njiani, akishuka, akiwa na amri mfukoni mwake, “Kukamata kundi hilo lote la watakatifu wanaojifingirisha,” hiyo ni kweli, “akifoka vitisho.” Mungu

akamwangusha kutoka kwenye farasi wake mrefu. Akamfanya shahidi wa kile walichokuwa nacho watu hao. Loo, jamani!

²³⁹ Sijui kama watu, usiku wa leo, hawampandi farasi yuyu huyu mrefu, usiku wa leo, wanapaswa kuangushwa, na kuwa shahidi.

²⁴⁰ Nimetazama asubuhi, wakati umande ungeshuka kutoka mbinguni. Nanyi angalieni jua linapochomoza, huo umande mdogo, uangalie jinsi unavyometa-meta kama tu nyota ndogo. Ni nini? Ni shahidi. Unajua, mara jua hilo linapochomoza kufikia mahali fulani, namna *hii*, linapochomoza kufikia mahali fulani, unapanda tena. Unyevu huo utapanda juu moja kwa moja. Kwa nini? Umekuwa huko juu wakati mmoja, nao ukaanguka tu. Unapanda tena. Ni shahidi wa mwanga huu wa jua, kuvuta juu. Umekuwa mahali fulani. Unajua yote yanahusu nini.

²⁴¹ Na kila mwanamume ama mwanamke aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu ni shahidi wa ufufuo wa Yesu Kristo. Jinsi Mungu anavyohitaji mashahidi wengine usiku wa leo! “Enendeni ulimwenguni mwote na mnishuhudie Mimi, kwa kila kizazi, kwa watu wote. Nitakuwa pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.” Roho Mtakatifu ayazamishe maneno haya machache kwenye kilindi cha nafsi yako. “Mtapokea Nguvu baada ya huyo, Roho Mtakatifu, akiwajilia juu yenu, nanyi mtakuwa mashahidi Wangu, katika Yerusalemu, Uyahudi, na hata pande za mwisho za dunia.”

²⁴² Wakati tukiinamisha vichwa vyetu; dada, waweza kuja kwenye kinanda? Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu, kila mahali, katika maombi. Kila mtu kwa uchaji uwezavyo sasa. Iweni katika maombi wakati wito wa madhabahuni unapofanywa. Roho Mtakatifu yuko hapa kila usiku, akitoa upako wa Kiungu, shahidi wa kufufuka kwake Yesu Kristo.

²⁴³ Sijui, usiku wa leo, kama uko hapa na ungependa kuwa shahidi wa Nguvu za kufufuka kwa Bwana? Wewe hujawahi kukaa mpaka ukavishwa Nguvu? Je, ungependa kukumbukwa katika maombi? Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mikono imeinuliwa, kila mahali, kwenye jengo. Loo, jamani! Hilo ni zuri sana.

²⁴⁴ “Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana hao watashibishwa.”

²⁴⁵ Je, kuna mtu yeyote ndani ya jengo, usiku wa leo, ambaye kamwe hajamkubali Kristo kama Mwokozi wake binafsi, ungesema, “Ndugu Branham, kwa mkono wangu ulioinuliwa. . . Madhabahu imejaa watu hapa sasa, lakini nitainua mkono wangu, kusema, niombeeni. Mimi ni mwenye dhambi. Na mimi—mimi hapa nataka sasa kumwacha Mungu auone mkono wangu, kwamba ninataka kumkubali kama Mwokozi wangu?” Mungu

akubariki, mama. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki. Mtu fulani upande wangu wa kulia? Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki huko juu. Hilo ni jema. Baadhi, huyu hapa mwingine. Mungu akubariki. Hiyo ni ajabu tu.

²⁴⁶ “Ninataka kuwa shahidi Wake”? Mwingine ambaye ungeinua mkono wako, na kusema, “Ndugu Branham, niombe. Ninataka kukumbukwa katika maombi”? Mungu akubariki. Ninakuona, mama hapo uliyeinua mkono wako, pia. Ninakuona wewe, kijana hapo mwishoni. Ninakuona umeinua mkono wako juu.

²⁴⁷ Mikono inainuliwa, kila mahali katika kusanyiko hili dogo usiku wa leo, kufungwa kwa uamsho. Tunajuaje. . . Huyu hapa mwanamke mwingine aliyeinua mikono yake. Mungu akubariki, dada. Unajuaje kama huu utakuwa ndio uamsho wa mwisho ambao Maskani ndogo ya Branham itawahi kuwa nao?

²⁴⁸ Nilisimama, leo, kule juu ya mwili baridi wenye barafu wa msichana mwenye umri wa miaka ishirini na kitu. Nikampeleka kaburini na kumzika. Wavulana wake wadogo walikuwa wameketi pale karibu na baba yao. Hao jamaa wadogo wakaenda hadi kwenye jeneza. Baba akasema, “Njoni, mwambieni mama, ‘Kwaheri.’” Wakaenda pale na kumpungia mikono yao midogo mama yao aliyekufa, aliyelala pale, “Kwaheri, mami.” Macho yao madogo ya hudhurungi yalifunikwa na machozi, nao walikuwa wameficha maskini nyuso zao mikononi mwao.

²⁴⁹ Loo, si ingekuwa huzuni ikiwa mama huyo angekuwa amekwenda milele? Lakini, kwa neema ya Mungu aliongokea hapa Maskanini. Usiku ule ambao alifanya uamuzi huo, na kwenda mbele, ndilo jambo pekee lililo na maana sasa. Juma lililopita alikuwa akizunguka huku na huku, mjini hapa, mwenye afya na mwenye nguvu, akitarajia kuja mkutanoni; akashikwa na ugonjwa, kisha akafa, muda mfupi tu.

²⁵⁰ Marafiki zangu wawili, wote walifanya kazi katika Kampuni ya Utumishi wa Umma, waligongwa jana katika ajali, wamelala hapa hospitalini, wanakufa sasa hivi, msichana yuafa. Nilifanya kazi pamoja naye, miaka kumi na saba; moyo ukapigwa ukarushwa upande wake mwingine. Mmoja wa waendeshaji wa kituo kidogo amelala pale, rafiki yangu; niliketi juu ya gogo, msituni, siku nyingi, na kuongea naye kuhusu Bwana Yesu. Ninataka kumwona katika muda mfupi tu sasa, nizungumze naye tena, kabla tu ya kutoka maishani. Nione kama Bwana atatwambia lolote kwa ajili yake.

²⁵¹ Nashangaa, wale ambao—ambao waliinua mkono wao, kuwa ni wenye dhambi, na walitaka kukumbukwa katika maombi. Umemkubali Kristo; sijui kama unaamini sasa kwamba unamkubali Yesu Kristo? Iweni katika maombi, kila mahali,

kila kichwa kimeinamishwa. Ukimkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wako binafsi, na kuamini kwamba alikuokoa kutoka dhambini, na sasa hivi ungeweza kusimama kwa miguu yako, kama shahidi. Mtu yeyote ambaye aliinua mkono wao, angesema, “Bwana, ninajua Wewe uliniahidi kwamba ‘Kila aaminiye hatahukumiwa.’ Sasa ninakuamini na kukubali Wewe kama Mwokozi wangu.”

²⁵² Je, utasimama? Tumbanwa kidogo na muda na nafasi hapa. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki. Endeeleni tu kusimama. Mkipenda, simameni. Je, mtu mwingine atasimama?

Mtu mwingine anasimama sasa hivi? Endeeleni tu kusimama, tafadhali. Kila mtu ainamishe kichwa chake sasa. Kila mahali humu jengoni, iweni katika maombi.

²⁵³ Bwana, saidia sasa. Ee Mungu, wasamehe wenye dhambi. Ulisema, “Yeye ajaye Kwangu, sitamtupa nje kamwe,” hawa ambao sasa wamesimama.

²⁵⁴ Mungu akubariki, ndugu. Endelea tu kusimama. Mtu mwingine? Baadhi yenu ambao mliinua mkono wenu, semeni, “Mungu, unirehemu, mwenye dhambi, na uniokoe kwa ajili ya Kristo.” Atafanya hivyo papo hapo, papo hapo. Filipino alisema . . .

“Haya hapa maji. Ni nini kinachotuzuia kubatizwa?” Filipino akasema, “Ikiwa unaamini kwa moyo wako wote, unaweza.”

²⁵⁵ Je, ungetaka kumkubali sasa hivi kama Mwokozi wako binafsi? Na ikiwa utasimama na kumshuhudia mbele ya watu, Yeye atakushuhudia mbele ya Baba yako na Malaika watakatifu. Anakutazama. Unataka kuwa shahidi? Simama kwa miguu yako, basi, kama wewe ni mwenye dhambi. Mungu akubariki, mama. Mtu fulani pale, mume na mke, waliteleza . . . huku wamekumbatiana, wanamkubali Kristo sasa kama Mwokozi wao binafsi. Mtu mwingine? Tafadhali simama kwa miguu yako, upesi sasa, wakati Roho Mtakatifu anapofanya kazi humu jengoni. Useme, “Ninataka sasa kumkubali Kristo kama Mwokozi wangu. Nataka uniombee.”

²⁵⁶ Hilo ndilo nitakalofanya, wakiwa wamesimama, huku machozi yakitiririka mashavuni mwao, jengoni. Je, utasimama? Tazama, kila mtu kwa uchaji, hakuna mtu anayesogea. Tafadhali iweni katika maombi.

²⁵⁷ Sikilizeni, Roho Mtakatifu sasa anawashughulikia watu. Ni nini kilikufanya uinue mkono wako? Hungeweza kuinua mkono wako isipokuwa Mungu amekufanya uinue. Yesu alisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba.”

²⁵⁸ Laiti ungejua, rafiki mwenye dhambi, kwamba watu ambao nimezungumza nao, wanaosema, “Simwamini Mungu. Sina wakati kwa ajili Yake. Wakati mmoja nilijaribu. Mimi . . . Hakuna . . . Hata sikuwa na shauku Yake.”

259 Na Mungu amekupa shauku, usiku wa leo. Kuwa Mkristo. Usimkatae.

260 Mpiga piano, mpiga kinanda, *Usimkatae*, tafadhali. Vema, unapofanya uamuzi wako.

Usimkatae, usimkatae,
Amerudi moyoni mwako tena,
Ingawa umepotea; (Bwana, naomba, hakika,
yeye...?...)

...katika Siku hiyo ya Milele!
Usimkatae Mwokozi moyoni mwako,
Usimkatae.

261 Loo, jinsi utakavyomhitaji, kusema, "Umefanya vema." Hivi hutasimama sasa na kusema, "Namkubali Kristo"?

262 Vipi kuhusu jambo hilo, dada, unaamini Yeye anakusamehe dhambi yako, unayesimama hapo?

Kila mtu mkiwa mmeinamisha vichwa vyenu. Tutafunga katika dakika moja.

263 Mkubali sasa, Yesu Kristo akibisha moyoni mwako. Hivi hutasimama na kusema, "Sasa ninamkubali Kristo kama Mwokozi wangu binafsi"? Hivi hutasimama kwa ajili ya maombi? Vipi kuhusu hilo, jamaa mdogo huko nje? Mungu akubariki. Mungu akubariki. Vipi kukuhusu wewe hapo nyuma, uliyeinua mkono wako, msichana? Si usimame sasa?

... unamhitaji akutetee
Katika Siku ile ya Milele!
Usimkatae Mwokozi moyoni mwako,
Usimkatae.

264 Wakati tukiimba pambio hilo tena. Sijui, kama wale waliosimama, wangeshuka moja kwa moja hapa, hebu niwape mkono na kuomba pamoja nanyi, papa hapa madhabahuni. Hivi mtakuja? Je, ninyi wengine hamtakuja? Vipi kukuhusu wewe uliyeinua mkono wako huko nyuma, mbona usije hapa? Njoo tu hapa chini. Mungu awabariki, mume na mke, shukeni hapa kwa dakika moja tu. Pandeni hapa juu. Ninataka kukupa mkono, ndugu, na wewe, dada.

... kurudi moyoni mwako...

Njoo pamoja naye, ndugu.


Ingawa umeenda mbali;
Ee jinsi utakavyomhitaji Yeye kuitetea kesi
yako
Kwenye hiyo...

Hivi hutakuja?

Usimkatae Mwokozi moyoni mwako,
Usimkatae.

²⁶⁵ Sasa, rafiki, wazia jambo hilo. Kabla ya asubuhi, huenda nafsi yako ikang'olewa kutoka mwilini mwako, kama jino linavyong'olewa, nje kupitia huko angani, kuingia kwenye Umilele usio na mwisho, itaenda. Katika ile Siku kuu, ya kuogofya ya Bwana, ni nani atakayeitetea kesi yako basi? Mbona usije? Kitu kidogo unachoweza kufanya katika siku hii ya ufufuo, ni kuja, useme, "Bwana Yesu, ninakuamini." [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²⁶⁶ . . .kuhubiri, na kuwasikia watu hawa wengine wakihubiri. Mungu yuko hapa, katika thibitisho, akisema, "Niliweka muhuri Wangu wa idhini juu Yake, ya kwamba ni Kweli." Ni Injili Yake. Wewe amini sasa, kwa moyo wako wote.

²⁶⁷ Nashangaa, tunapotoa wito, kama kuna mtu aliyerudi nyuma hapa, angesema, "Ndugu Branham, nikumbuke, sasa hivi. Nikumbuke. Ninainua mkono wangu. Nikumbuke katika maombi"? Angalia, moja ya siku hizi, utaaga, ukamkabili Yesu Kristo. 

MASHAHIDI SWA53-0405E

(Witnesses)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili ya Pasaka jioni, tarehe 5 Aprili, 1953, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org